**SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALI MBALI NA KUWEKA MASHARTI BORA NDANI YAKE**

---

**MPANGILIO WA VIFUNGU**


| VIFUNGU | MAELEZO |
| --- | --- |

**SEHEMU YA KWANZA**
**MASHARTI YA AWALI**

1. Jina fupi na kuanza Kutumika.

2. Marekebisho ya Sheria mbalimbali.

**SEHEMU YA PILI**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA MAHAKAMA YA BIASHARA ZANZIBAR (DIVISHENI YA MAHAKAMA KUU), NAM. 9 YA 2013**

3. Kusomwa.

4. Marekebisho ya kifungu cha 7.

5. Marekebisho ya kifungu cha 28.

**SEHEMU YA TATU**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA MAJI NA NISHATI ZANZIBAR, NAM. 7 YA 2013**

6. Kusomwa.

7. Marekebisho ya kifungu cha 24.

8. Kuongezwa kifugu kipya cha 24A.

**SEHEMU YA NNE**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA UTAWALA WA BARAZA LA WAWAKILISHI, NAM. 6 YA 2019**

9. Kusomwa.

10. Marekebisho ya kifungu cha 14.

11. Marekebisho ya kifungu cha 19.

**SHERIA NAM. 9 YA 2019**

**NIMESAINI**

**{DKT. ALI MOHAMED SHEIN}**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

30 Disemba, **2019**

# SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALI MBALI NA KUWEKA MASHARTI BORA NDANI YAKE

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza Kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbali mbali, 2019 na itaanza kutumika mara baada ya kutiwa saini na Rais.

Marekebisho ya sheria mbalimbali.

**2.** Sheria zilizotajwa katika sehemu mbali mbali za Sheria hii zinarekebishwa kwa namna zinavyoelezwa katika sehemu husika.

## SEHEMU YA PILI
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA MAHAKAMA YA BIASHARA ZANZIBAR (DIVISHENI YA MAHAKAMA KUU), NAM. 9 YA 2013

Kusomwa.

**3.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Mahakama ya Biashara Zanzibar (Divisheni ya Mahakama Kuu) Nam. 9 ya 2013 ambayo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 7.

**4.** Kifungu cha 7 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuongeza vifungu vidogo vya (4) na (5) kama ifuatavyo:

"(4) Mjumbe wa Kamati atashika madaraka kwa kipindi cha miaka mitatu na anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine kimoja".

"(5) Jaji Mkuu anaweza, kila baada ya muda, kupendekeza posho za vikao na maslahi mengine ya Wajumbe wa Kamati kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma, kanuni na miongozo".

Marekebisho ya kifungu cha 28.

**5.** Kifungu cha 28 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kufuta kifungu kidogo cha (1) na badala yake kuweka kifungu kidogo kipya cha (1) kama ifuatavyo:

"(1) Bila ya kujali sharti lolote chini ya Sheria hii, endapo Jaji anayeendesha kesi ataona ni lazima uendeshaji wa kesi ufanywe kwa msaada wa washauri, Mahakama itawaalika washauri kutoka katika orodha iliyowasilishwa na Kamati ya Watumiaji wa Mahakama ya Biashara".

(b) kuongeza kifungu kidogo kipya cha (3) mara baada ya kifungu kidogo cha (2) kama ifuatavyo:

"(3) Endapo katika uendeshaji wa kesi mshauri mmoja hatahudhuria, Mahakama inaweza kuendelea na kuihitimisha kesi hiyo na mshauri aliyebakia".

## SEHEMU YA TATU
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA MAJI NA NISHATI ZANZIBAR, NAM. 7 YA 2013

Kusomwa.

**6.** Sheria hii itasomwa pamoja na Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar Nam. 7 ya 2013, ambapo katika Sheria hii itajulikana kama "Sheria mama".

Marekebisho ya kifungu cha 24.

**7.** Kifungu cha 24 cha Sheria Mama kinafutwa na kuwekwa badala yake kifungu kifuatacho:

Mapato kuwekwa katika hesabu za Serikali.

**24.** Mapato yote yaliyokusanywa au kulipwa kwa Mamlaka chini ya Sheria hii au sheria nyengine yoyote, yataingizwa katika hesabu za Serikali kwa mujibu wa taratibu za fedha za Serikali.

Kuongezwa kifungu kipya cha 24A.

**8.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 24A mara baada ya kifungu cha 24 kama ifuatavyo:

Fedha za Mamlaka.

24A. Fedha za Mamlaka kwa ajili ya kusimamia kazi zake zitajumuisha:

(a) kiwango kinachoweza kupatikana kwa njia ya kubakiza asilimia ya mapato yaliyokusanywa na Mamlaka kama itakavyoamuliwa na Waziri anayehusika na fedha kila baada ya muda; na

(b) kiwango kinachoweza kupokelewa au kilichopatikana na Mamlaka kwa njia ya msaada, mkopo, michango, ada au fedha nyengine kwa madhumuni ya utekelezaji wa kazi zake baada ya kuidhinishwa na Waziri.

## SEHEMU YA NNE
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA UTAWALA WA BARAZA LA WAWAKILISHI, NAM. 6 YA 2019

Kusomwa.

**9.** Sheria hii itasomwa pamoja na Sheria ya Utawala wa Baraza la Wawakilishi, Nam. 6 ya 2019, ambayo katika Sheria hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 14.

**10.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kufutwa aya ya (h) katika kifungu cha 14(1).

Marekebisho ya kifungu cha 19.

**11.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kufutwa aya ya (e) katika kifungu cha 19(2).

**UMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 28 Novemba, 2019.

..........................................

(RAYA ISSA MSELLEM)

***Katibu wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.***